

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Tatu – Tarehe 3 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge leo hatutakuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Katibu!

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tunaanza na Wizara ya Nishati namwita Mhe. Dkt. Daniel Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki aulize swali lake.

Na. 17

**Umeme wa REA Kuunganishwa Kata zisizo na
Umeme - Arumeru Mashariki**

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO Aliuliza:-

Je, lini Serikali itawaunganishia umeme wa REA wananchi wa Vijiji vilivypopo katika Kata za Jimbo la Arumeru Mashariki ambazo hazina umeme?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Arumeru Mashariki lina jumla ya Kata 26 na vijiji 90. Ni vijiji 12 tu ambavyo havina umeme na sasa vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaoteklezwa katika Jimbo la Arumeru Mashariki. Kazi zinazofanyika sasa ni usanifu wa kina, upimaji, uandaaji wa michoro na manunuzi ya vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unahuisha ujenzi wa njia za umeme ya msongo kilovoti 33 zenyе urefu wa kilomita 40.30; kilomita 12 ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4; ufungwaji transfoma 12 za KVA 50; pamoja na kuunganisha wateja wa awali 264. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 2.071 na utekelezaji wake unatarajiwа kukamilika Mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine Serikali imefanya uhakiki na kuainisha uwepo wa vitongoji takriban 37,610 visivyokuwa na umeme Tanzania Bara na inakadiriwa kuwa shilingi trillion 7 zitahitajika ili kukamilisha mahitaji ya umeme katika vitongoji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishaanza utekelezaji wa miradi ya ujazilizi unaolenga kufikisha umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwa ni pamoja na Vitongoji vya Jimbo la Arumeru Mashariki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pallangyo swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili niliuliza kwa sababu kuna kata nyingi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

sana kule ambazo hazijapata umeme hususani Kata ya Uwilo kuna vijiji kama viwili vile Lukulu Skimosoni na kule Maruhango pia kuna vijiji maruhango kwenye hakuna umeme je, niulize ni lini hasa vijiji hivyo vitapata umeme?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Pallangyo na nimshukuru kwa ufuatiliaji na uvumilivu kwa sababu jumbo lake ni moja ya majimbo ambayo mkandarasi alichelewa kupatikana kwa sababu ya taratibu ya kimanunuzi. Lakini kama nilivyosema kwenye swali na jibu la msingi ni kwamba kufikia Disemba mwaka huu kwa mujibu wa mkataba kata zote ambazo haziha umeme ambazo ni vijiji kwakwe ni vijiji 12 ndiyo havina umeme vitakuwa vimepatiwa umeme kwa kadri ya mkataba tuliokuwanao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilini Serikali itajenga *substation* ya kule Mkuranga sambamba na kuweka *transformer* ya NVA 90 pale katika *substation* ya Mbagala ili kuondoa tatizo la ukatikaji wa umeme mara kwa mara katika jumbo la Mbagala?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jumbo la Mbagala linalo *substation* ndogo kama alivyosema ambayo ina *transformer* yenye uwezo wa AVA 50 NA *substation* hiyo inapeleka umeme mpaka maeneo ya mkulanga na kwa bahati nzuri ambayo inakuwa mbaya kwa upande mwagine. Eneo la Mkulanga limekuwa na viwanda vingi sana na hivyo linachukua umeme mwangi sana kutoka eneo la Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza upembuzi wa kujenga kituo cha kupoza umeme eneo la

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mkulanga ambacho kitakuwa kina zaidi ya Megawatt 100 lakini taratibu za kukamilisha ununuzi wa *transformerya* AVA 90 itakayokuja kufungwa pale Mbagala zinakamilika na tunaamini kabla yam waka huu kuisha kituo cha Mbagala kitakuwa kimeongezewa uwezo wakati kule Mkulanga *substation* ikiwa inapatikana fedha kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Joseph Mkundi Mbunge wa Ukerewe

MHE. MICHAEL J. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na sinto fahamu kubwa juu ya kiwango gani kitozwe kwa wananchi ili kuweza kuvutiwa umeme kwenye maeneo mbalimbali wakiwemo wananchi wa eneo la Nasio Wilaya Ukerewe. Nilitakakujua ni vigezo gani vinavyotumika kujua ni kiwango gani cha pesa kinatakiwa kulipwa na mwananchi ili aweze kuvutiwa umeme kwenye eneo lake la nyumba.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Byabato majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mkundi kwa swali lake nzuri Mbunge wa Ukerewe ambaye pia amekuwa akifuatilia sana mambo ya umeme katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka tulikuwa tume *standardize* gharama za upatikanaji wa umeme lakin baadaye tulimuomba Mheshimiwa Rais atukubalie tufanye marekebisho katika baadhi ya maeneo ili kuweza kufanya kazi hii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumerudi kwenye vile viwango ambavyo tulikuwa tunavitumia hapo awali ambapo maeneo ya mijini yanapata umeme kwa gharama ambazo wenzetu wa EWURA ndiyo wa simamizi wa gharama wameziweka zinaanza laki tatu na kuendelea. Lakini maeneo ya vijiji yanapata umeme kwa gharama ya shilingi elfu saba

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwa *line* ya njia moja na gharama nyingine zile za kawaida kwa njia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango na vigezo ambavyo tunavitumia viko katika sheria ya mipango miji ile ndiyo inayosema hapa ni jiji hapa ni mji hapa ni Kijiji na hapa ni nini. Kwa hiyo, kwa kutumia sheria hiyo ambayo inatumwa na wenzetu wa TAMISEMI na watu wa ardhi tunaitumia hiyo sasa *ku-decide* kwamba hapa itakuwa 27 hapa itakuwa zile gharama za mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajipanga kuendelea kutoa elimu kubwa Zaidi ili wananchi waweze kuelewa kwamba kiwango gani kinatozwa wapi na kwa sababu zipo kwa mfumo huo niliousema kwa hapo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri tunakwenda Ofisi ya Rais TAMISEMI, namuita Hussein Nassor Mbunge wa Nyang'hwale aulize swali lake.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo Nyang'hwale, wakishirikiana na Mkoa wa Geita, Geita ya dhahabu utajiri na heshima kwa kumpongeza Mheshimiwa Spika Dkt. Tulla Ackson kwa kuitishwa kwa kura nyingi za kishindo, hongera sana Mheshimiwa. Sasa swali langu namba 16 lipate majibu ya Serikali. (*Makofii*)

Na. 16

Hitaji la Watumishi wa Afya Nyang'hwale

MHE. HUSSEIN N. AMAR Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi katika Vituo vya Afya vya Kharumwa na Nyang'hwale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)
Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassor Hussein Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha upatikanaji wa watumishi wa kada za Afya katika Vituo vya kutolea huduma za Afya ili kuendana na upanuzi wa miundombinu ya Afya ya Msingi nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali iliajiri watumishi 2,726 wa kada mbalimbali za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika ajira hizo za Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ilipangiwa watumishi 20 ambapo Kituo cha Afya Kharumwa kilipata watumishi 3 na Kituo cha Afya Nyang'hwale kilipata watumishi 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri na kugawa watumishi kwenye Halmashauri na Vituo vya kutolea huduma za Afya kadri ya upatikanaji wa vibali vya ajira na fedha ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassor Amar swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyonge kwanza niipongeze Serikali kwa kutupatia watumishi 20 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 watumishi watatu kituo cha afya Karumwa na wanne kituo cha afya Nyang'ahwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 kutokana na upungufu uliopo katika vituo vyetu vya Nyang'gwale ambavyo sasa hivi wilaya hiyo imekuwa na mfumuko mkubwa wa madini na watu wengi wamejazana katika wilaya hiyo huduma bado inaitajika sana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwenye kituo cha afya kama vile wilaya Je, Serikali iko tayari kutuungezea watumishi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha nydingi katika sekta ya afya na kuweza kukamilisha zahanat zaidi ya 10 ambazo tunatarajia kuzifungua hivi karibuni. Je, Serikali imejjipanga vifaa tiba na watumishi ili tuweze kuanzisha huduma katika zahanati hizo 10.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange Naibu Waziri TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nassor Hussein Amar Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee pongezi zake nydingi kwa Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika sekta ya afya. Lakini nimuhakikishie katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 kuna vibali vya ajira ambavyo vitatolewa ili kuajiri watumishi kwenda kupunguza upungufu wa watumishi katika vituo vyetu vya afya kote nchini vikiwepo vituo vya afya katika halmashauri na Jimbo hili la Nyang'hwale. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Jimbo la Nyang'hwale katika vituo hivi vitapewa kipaumbele katika ajira inayokuja ili kuhakikisha tunapeleka watumishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ni kweli kwamba tumeendelea kujenga vituo vingi katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na Serikali imeshafanya tathimini tunajumla ya vitu 1073 ambavyo tunatarajia ifikapo Juni mwaka huu vitakuwa vimekamilika na vitahitaji vifaa tiba, vitahitaji watumishi na tathimini imeshafanya na maandalizi ya kupata vifaa tiba hivyo na watumishi imeshafanya kwa hiyo iliyobakia ni suala

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

la utekelezaji. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba vituo vyetu ambavyo vinaendelea kujengwa tayari tathimini inajulikana na kazi yakupeleka watumishi na vifaa tiba itakwenda kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: nimekuona Mheshimiwa Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoa na shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa fedha tulizopata kwa kujenga vituo vya afya Pamoja na kukarabati kituo cha kule Kirua Vunjo na Marangu *headquarter*. Nina swali kuhusu kituo ambacho tumeahidiwa pale *OPD* Himo mji mdogo wa Himo. Kituo hiki kinahudumia watu wengi sana watu zaidi ya 36 elfu lakini bahati mbaya hakina majengo ya upasuaji, mahabara na Mochwari na tulipoahidiwa hili jambo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa afya wakati wa kampeni tulijua kwamba tutafanyika na imefanyika lakini haya majengo hayapo. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, ni lini tutapata fedha kwa kujenga majengo haya ili kituo hiki sasa kiweze kutumika na kutoa huduma zote zinazostahili kwa kituo cha afya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunavituo vingi nchini vikiwepo vituo vya Jimbo Vunjo ambavyo kwanza vinamiundombinu michache kulinganisha na huhitaji wa vituo vya afya ikiwemo majengo kama mahabara majengo ya upasuaji lakini pia upungufu wa mawodi. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo cha afya cha OPD himo ni mionganoni mwa vituo ambavyo tumeviahinisha na tumeviwekea mpango kazi wa kutafuta fedha ili kwenda kujenga majengo hayo ambayo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

yatavifanya vikamiliike kuwa vituo vya afya na hatimaye viweze kutoa huduma zile ambazo zinatarajiwa. Kwa hiyo, tunatafuta fedha Mheshimiwa Mbunge na niwahakikishie kwamba fedha ikipatikana tutawapa kipaumbele kitu cha afya cha *OPD* Himo.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Kasalali Mageni Mbunge wa Sumve.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ilivyo maeneo ya Jimbo la Nyang'hwale inafanana na kabisa na hali ilivyo kwenye Jimbo la Sumve ambalo lina Kituo cha Afya cha Nyambiti ambacho kilibadilishwa kilikuwa zahanati na kituo hicho cha afya kina hudumia kata 13 za Jimbo la Sumve ambazo zina wakazi zaidi ya laki mbili na kituo kile hakina majengo kama ya upasuaji mahabara na majengo ya muhimu ambayo yangesaldia katika kutoa huduma stahiki ya afya kwa watu wale. Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha watu wa Jimbo la Sumve katika kituo cha afya cha nyambiti na wenyewe wanapata huduma nzuri kama ilivyo katika vituo vingine vya afya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Kasalali Mageni Mbunge wa Jimbo la Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika halmashauri zetu na katika majimbo yetu tuna vituo vya afya ambavyo vina majengo pungufu kama nilivyotangulia kujibu katika jibu langu lilitopita na mpango wa Serikali ni kuhakikisha *standard* ya vituo vya afya inafikiwa kwa maana ya kuwa na majengo yale yote ya muhimu yanayofanya kituo kile kiwe na hadhi ya kuwa kituo cha afya. Kwa hiyo, kuwepo kituo hiki cha afya cha Nyambiti katika jimbo hili Mheshimiwa Mbunge naomba nimuhakikishie kwamba tutafanya tathimini pia kuona umetupa taarifa kwamba hakuna majengo ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

upasuaji na mahabara na tunajua ni muhimu na yanahudumia zaidi ya kata 13 ni moja ya kituo cha afya cha kimkakati na ninajua ulikihainisha kwa hiyo tukitafuta fedha tutahakikisha tunaipa kipaumbele kujenga majengo hayo ili wananchi wale wote wapate huduma bora za kituo cha afya.

MWENYEKITI: Namuita Mheshimiwa Flatei Gregory Massay aweze kuuliza swali lake.

Na. 18

Ahadi ya Kupeleka Umeme kwenye Vijiji na Vitongoji – Mbulu Vijijini

MHE. FLATEI G. MASSAY Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Jimbo la Mbulu Vijijini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WAZIRI WA NISHATI Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu vijijini lina jumla ya vijiji 76 na vitongoji 362. Ni vijiji 42 tu ambavyo havina umeme katika Jimbo la Mbulu Vijijini na sasa vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaotekelawa katika Jimbo hilo. Kazi zinazofanyika sasa ni manunuzi ya vifaa na ujenzi wa miundombinu ya umeme. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika hatua nyingine Serikali imefanya uhakiki na kuainisha uwepo wa vitongoji takriban 37,610 visivyokuwa na umeme Tanzania Bara na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

inakadiriwa kuwa shilingi trillion 7 zitahitajika ili kukamilisha mahitaji ya umeme katika vitongoji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishaanza utekelezaji wa miradi ya ujazilizi unaolenga kufikisha umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwa ni pamoja na Vitongoji vya Jimbo la Mbulu Vijijini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanzu nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuja kuzindua umeme katika Jimbo la Mbulu Vijijini. Lakini nataka nimtaarifu kwamba pamoja na kuja kuzindua ule umeme baada ya kuondoka hakuna kilichoendelea, maana yake mkandarasi hayuko *site*.

Je, atafanya nini ili walau mkandarasi yule arudi *site* aweze kuendelea kuunganisha vile vijiji ambavyo mkandarasi amesaini kama mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ziko kata ambazo kwa kweli zina hali mbaya na uliahidi kwamba umeme utafika; ni lini hasa zile kata ambazo wewe mwenyewe alitamka wakati anazindua umeme Mbulu Vijijini zitapata umeme? Maana sasa hivi kama nilivyosema, wakandarasi hawako *site*. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimpongeze Mheshimiwa Massay kwa sababu kweli tulikwenda kuzindua umeme katika jimbo lake na tulizindua umeme katika Kijiji kinachoitwa Munguhai, ni eneo zuri sana, na uwepo wa Mungu ulionekana kweli katika kijiji hicho.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mkandarasi anapopewa kazi ya *REA* kuna awamu kama nne za kufanya. Baada ya kusaini mkataba mkandarasi anakwenda *site* kufanya *survey* ili kubaini kama ile kazi ilioandikwa kwenye karatasi ndiyo hasa ile ya kufanyika kazini. Na hiyo mara nyingi inachukua miezi mitatu mpaka mitano kulingana na hali ya hewa, eneo linavyofanana na wigo wa upana wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linafanyika baada ya hapo, wanakwenda kufanya uhakiki watu wa *TANESCO*, *REA* pamoa na mkandarasi mwenyewe, wanashirikiana kuona kama kilichoonekana *site* endicho hicho hasa ambacho kinatakiwa kifanyike na wanakubaliana. Baada ya hatua hiyo, inakwenda sasa kwenye ununuzi wa vifaa. Baada ya vifaa kupatikana ndiyo sasa tunakwenda kwenye utekelezaji wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi hatua tatu nilizozitaja za kwanza za *survey*, kwenda kwenye kufanya uhakiki na ununuzi wa vifaa unachukua miezi nane mpaka kumi kukamilika. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, najua kwenye maeneo mengi hatua hizi ndiyo sasa zinalekeea kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi sana ambapo wakandarasi watakuwa hawaonekani *site*, siyo kwamba wame-*abandon site*, hapana, watakuwa kwenye moja wapo ya hizo hatua ambapo pengine hawaonekani kuwepo sana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwahakikishie kwa maelekezo yaliyokuwepo mikataba yote inatakiwa ikamilike Desemba mwaka huu na tunatarajia kuanzia mwezi Machi mwanzoni wakandarasi wengi watakuwa wamemaliza zile hatua za manunuzi na *surveyna* watakuwa wamefikisha vifaa *site* wataanza kuonekana wakifanya kazi kwa miezi nane mfululizo ili kazi hizo ziweze kukamilika kwa wakati. Kwa hiyo na ndugu yangu, Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Vijijini atakuwa kwenye *category* hiyo hiyo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye eneo la pili kama nilivyosema tangu mwanzo, vijiji vyote ambavyo havina umeme vitapatiwa umeme kabla ya Desemba na vijiji vingine vilivyopo kwenye kata alizotajta vikiwemo. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa George Mwenisongole.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kuna mkanganyiko mkubwa kuhusu bei ya umeme vijijini; kwa nini Serikali isitoe tamko hapa Bungeni ili wananchi wote wanaoishi vijijini waelewe bei ya umeme vijijini ni shingapi, ni shilingi 27,000 au ni hiyo 300,000? Ili kuondokana na sintofahamu inayowapata wananchi wa vijijiji.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mwenisongole kwa swali lake zuri na kwa ufuatiliaji wa mambo yanayowahusu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatoa tamko na mimi nillirudie; umeme vijijini ni shilingi 27,000 kwa njia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena; kwa *single phase* vijijini umeme ni shilingi 27,000. Ilikuwa jana na itakuwa leo na kwa hali ilivyo sasa na maelekezo tuliyonayo itakuwa hivyo kesho, shilingi 27,000. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakagenda nimekuona.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo shida ya vitongoji vya Mbulu, katika Wilaya ya Rungwe Kitongoji cha Ngana kina wakazi wapatao 600, lakini walionunganishiwa umeme wa REA ni familia 36 tu peke yake; ni nini Serikali inajipanga kwenda kuhakikisha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

vitongoji vile na familia zingine zinapata umeme kama wanavyopata wananchi wengine?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri, naona amesimama Mheshimiwa Waziri wa Nishati; karibu Mheshimiwa January Makamba.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, kwa majibu mazuri ambayo aliyatoa awali katika maswali yaliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nizungumzie hili suala la vitongoji kwa sababu hii changamoto ipo karibu katika kila jimbo, kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kupeleka umeme katika vijiji karibu vyote, na tunavyo vijiji 12,345 hapa nchini na takribani vijiji vyote tutavimaliza itakapofika Desemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika vijiji hivyo tuna vitongoji 64,760, na katika vitongoji 64,000 vitongoji 37,610 havina umeme. Kwa hiyo, vitongoji zaidi ya asilimia 58 havijafikiwa na umeme wakati vijiji zaidi ya asilimia 80 vimepata umeme. Na tunafahamu kwamba manufaa ya umeme siyo unapofika kijijini, ni pale unapowafikia watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetazama mahitaji ya kupeleka umeme katika vitongoji vyote, ni karibu shilingi trilioni 7.4, na tumeangalia mahitaji ya urefu wa nyaya, idadi ya transfoma na kila kitu ili tuweze kufanya kazi hii ya kupeleka umeme katika vitongoji vyote kwa muda mfupi. Ndiyo kazi ambayo nilikuwa nimefanya tangu niingie katika nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ni fedha. Kwa utaratibu wa tunavyopata fedha za *REA* sasa hivi itachukua miaka 23 kumaliza vitongoji vyote. Sasa ndani ya Serikali tumetafakari na tumekuja na *options* tatu na hapo mbele tutaamua ni ipi twende nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *option* ya kwanza ni hii ya sasa hivi tunayoendelea nayo ambayo itachukua muda mrefu, kama miaka 23. *Option* ya pili ili tufanye ndani ya miaka minne lazima tutenge bajeti karibu shilingi triliuni 1.8 kila mwaka kwa kazi hiyo. *Option* ya tatu ni kutoa hati fungani ya nishati vijiji (energy bond) ambayo mapato ya mafuta, ile *petroleum levy* ya shilingi 100, tunai-ringfence kwa miaka 20 ambayo itatupa karibu dola bilioni 3.1 na hiyo *bond* tunaipeleka sokoni, hizi fedha zote tunazipata sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tukubaliane kwamba *charge* ya mafuta tutai-peg kwenye dola, hiyo shilingi 100 kwa miaka 20. Na matumizi ya sasa hivi ya mafuta ni lita milioni 10 kwa siku, kwa hiyo kwa miaka 20 – na tunaamini matumizi yataongezeka – kwa miaka 20 kwa hakika kabisa tutapata pesa za kulipa hiyo hati fungani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *option* ya tatu ni kitu wanaita *EPC plus F, Engineering, Procurement, Construction plus Financing*, kwamba kampuni kubwa zinazoweza kupeleka umeme vijiji kwa mkupuo kwenye vitongoji zinakuja na *proposal* lakini na *financing* ambayo ni concessional; asilimia moja kwa miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba katika kutafakari hizo *options* tunaweza tukapata ambayo itakuwa ni nafuu kwa maana ya *interest*, lakini itatuwezesha kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote kwa kipindi cha miaka minne. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakapokamilisha kufanya kazi hilo jambo tutakuja Bungeni na kuwaeleza ni *option* ipi ambayo tumekwenda nayo. Na tutakapoamua kwa hakika kabisa dhamira yetu sisi ni kwamba Wabunge hapa watakapokuwa wanaelekea kwenye uchaguzi basi umeme lisiwe jambo ambalo litawaangusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na maelekezo hayo tumepewa na Mheshimiwa Rais, na katika kipindi hiki kifupi tutakuja na *plan* ya *financing* ya kupeleka umeme kwenye

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

vitongoji 37,000 katika kipindi cha miaka minne ili tuisubiri miaka 20. Kwa hiyo, naamini kabisa maswali yote ya umeme vitongojini yatakuwa yameisha mara tutakapokuja na hiyo *plan*. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa majibu ya maswali yanayoulizwa sana kuhusu umeme vitongojini na umeme kwenye taasisi za Umma huko vijijini.

Naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Itigi aulize swali lake la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itupe ufanuzi kidogo; pamoja na ufanuzi uliotolewa wa shilingi 27,000 katika vijiji lakini kabla ya hapo kulikuwa na bei tatu; kulikuwa na 320,000; 177,000 kwenye vimiji vidogo kama Itigi na 27,000 kwa vijiji. Sasa wametoa wale wa 177,000 wamewapeleka kwa 320,000; vijiji ambavyo vimeungana vijiji vitatu vinne kwa kuwa tu vina kasoko basi vinaonekana ni mji vilipe 320,000/-. Je, Serikali iko tayari sasa kukubaliana na bei zilizokua kabla ya kurudi 27,000 na kuwa 177,000 kwa mji midogo? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri kutoka kwa Mheshimiwa Massare. Ni kweli hata kabla ya hapa tayari sisi kama Wizara kwa niaba ya Serikali tumeshapata mapendekezo na maoni na maombi mbalimbali ya ku-varyhizi gharama ambazo tuko nazo sasa. Na wengine wakaenda kwenye kupendekeza kwamba hata mtumishi wa Umma anavyolipwa posho anapoenda kwenye jiji, manispaa au wilaya, zile posho anazopewa zinatofautiana.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali niseme tumelipokea na tutakwenda kulifanyia kazi ili kuangalia uhalisia wa maisha tunayoishi sasa na gharama ambazo Serikali inaweza ikazitoza ili wananchi waweze kupata huduma hii ya umeme kwa gharama nafuu ambayo inamfikia kila mtu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambapo *REA* wamepeleka umeme wamepitisha laini kuu na pale chini kwa wananchi wa kawaida hakuna umeme. Kwa mfano nimueleze Mheshimiwa Waziri, nina vitongoji 610, vitongoji ambavyo havijafikiwa ni 503 na ukija kuangalia wanasema vijiji karibu asilimia zaidi ya 75 vimeshapata umeme, lakini ukiangalia wananchi wengi hawana umeme na mahitaji ni makubwa. Ni lini hivi vitongoji vitapelekewa umeme? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na ninamshukuru kaka yangu, Mheshimiwa Bilakwate, kwa swali zuri kabisa, na mimi Kyerwa ninapafahamu. Lakini ninaomba Mheshimiwa Bilakwate achukue tu na kuamini maeleo aliyojatoa Mheshimiwa Waziri, kwamba tunafahamu kwamba vitongoji vingi sana havina umeme na *plan* na mkakati mkubwa sana wa Serikali wa kufikisha umeme katika vitongoji hivyo vyote ndani ya miaka minne upo na unaendelea na utakapokuwa tayari vitongoji vyote 37,000 nchini ambavyo havina umeme vitapatiwa umeme.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa tunakwenda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, namuita Mheshimiwa Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 19

NGO's Kupata Rasilimali Fedha Ikiwemo Ruzuku

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA Aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuja na mpango mkakati wa kuwezesha *NGOs* kupata rasilimali fedha kuititia njia mbalimbali ikiwemo ruzuku katika maeneo mahsus kama ambavyo inafanya kwa Vyama vya Siasa, hasa baada ya uamuvi wa Serikali kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambayo inahusisha Asasi za Kiraia katika malengo yake?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM Alijibu: -

Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante sana. awali ya yote kwa ridhaa yako naomba niseme maneno machache tu kwa sababu hii ni Wizara mpya.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kutoa shukrani zangu za pekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake makubwa ya kuunda Wizara hii mpya itakayoshughulikia masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalum.

Mheshimwa Mwenyekiti, hakika maono yake yamekuja kwa wakati ambapo kwa sasa kasi ya maendeleo kuititia msukumo wa teknolojia ni kubwa na changamoto za nchi yetu ni nyingi katika makundi mbalimbali ya jamii zetu, jambo ambalo linahitaji chombo mahususi cha kuangalia kwa kina zaidi changamoto hizi na fursa zilizopo ili kuweza kuiendeleza jamii yetu.

Mheshimwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru kwa imani yake kwangu kuendelea kuniamini na kunitueua niweze kuisimamia Wizara hii. Mimi na timu yangu yote ambayo ametuamini tunaahidi hatutamuangusha. Tutaungana na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

jamii na wadau wote kuhakikisha tunaleta msukumo wenye tija kuendeleza maono aliyonayo na jamii yetu kuweza kuendelea na kuwa na ustawi.

Mheshimwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nijielekeze kwenye swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum. Majibu ya swali hili ni kwamba: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa hajitatenga fungu maalum kwa ajili ya ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hata hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mashirika hayo kuwa uendelevu, tarehe 30 Septemba, 2021 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliagiza Wizara kwa kushirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali kuandaa Mpango Mkakati wa kuwezesha mashirika haya kupunguza utegemezi. Rasimu ya andiko la awali la Mpango huu imeandaliwa ambayo imeainisha njia mbalimbali za kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuweza kupata rasilimali za kutekeleza shughuli zao. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Lugangira nimkuona, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami niungane na Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya sekta ya Asasi za Kiraia, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda Wizara hii mpya mahususi ambayo inalenga kusimamia masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, na kwa kuwa tunafahamu sisi waswahili tunasema anayemlipa mpiga zumali ndio anayechagua wimbo, sasa kwa mustakabali huo na kwa kutambua kwamba *NGOs* nyingi zinapata fedha ambazo zimetengwa na Serikali za nje; je, Serikali haioni ipo haja ya kuona namna gani ambavyo pia itatenga fedha kwa ajili ya *NGOs* za ndani ili kuepusha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

baadhi ya *NGOs* kwenda na kufanya kazi ambazo zinakwenda kinyume na maadili na malengo ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa hali ya sasa ipo changamoto kubwa sana kwa upande wa *TRA* na namna ambavyo inaangalia hizi *NGOs*. Pale ambapo inatokea *NGO* inapata rasilimali fedha na inakwenda kutekeleza mpango ule kutoka mwaka mmoja kwenda wa pili, *TRA* wanatoza kodi ya mapato kwenye hizi *NGOs* kwenye zile fedha ambazo zinakuwa zimebaki mwisho wa mwaka, lakini zinakwenda kutekeleza mradi mwaka unaofuata. Nwa kwa mantiki hiyo *TRA* inafanya hivyo kana kwamba *NGOs* zinafanya biashara wakati hazifanyi biashara, zinatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Serikali haioni haja ya kuleta hizì sheria, kanuni na haya maelezo mbalimbali ambayo yanatoa fursa kwa *TRA* kufanya hivyo ili iletwe Bungeni ifanyiwe maboresho ili kuimarisha mazingira wezeshi kwa hizi Asasi za Kiraia ili ziweze kuendelea kufanya kazi kwa tija na kuendelea kuchangia maendeleo ya jamii ambayo kimsingi ili Wizara hii itekeleze malengo yake ni lazima ifanye kazi kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia? Ahsante. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa nyingine niweze kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, Neema Lugangira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sehemu ya kwanza, kwamba Serikali ina mpango wa kutoa fedha kwa ajili ya Mashirika haya Yasiyo ya Kiserikali. Niseme kwamba Serikali imekuwa ikifanya hivyo tangu miaka ya nyuma kwenye baadhi ya taasisi chache ile zile *NGOs* ziweze kuchangia maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni *CCBRT*, ile ni hospitali yetu ambayo inawanufaisha akinamama na watoto na watu wengine wenye magonjwa mbalimbali ya ulemavu. Imekuwa ikipeleka fedha kule tangu miaka ya 2000 na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kikubwa katika mwelekeo huo, pamoja na hili andiko tunalolifanya kazi, bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali inajielekeza kuanza kutekeleza mpango wa ruzuku kwenye baadhi ya hizo *NGOs* zitakazokuwa zimeonekana zina vigezo na tutawasilisha kwenye kipindi cha bajeti, mtaweza kuona mwelekeo huo wa Serikali.

Mheshimwa Mwenyekiti, aidha, katika kipengele kingine cha pili cha swali, maboresho ya kanuni na sheria ili kuzifanya hizi *NGOs* zetu ziweze kufanya kazi kwa kujiamini na kuwa na uendelevu baadaye. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu alishaelekeza, andiko limeanza kuandikwa lakini tayari tumeanza kutekeleza kupata maoni kutoka kwenye *NGOs* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilifanyika kikao Arusha; Mashirika 200 yalikaa yakatoa maoni na tarehe 5, hapa Dodoma kinafanyika kikao kingine, *NGOs* nyingine zimealıkwa, zitakuja kutoa maoni na baadaye tunakwenda Mwanza Kanda ya Ziwa, tunafunga. Yale maoni ndiyo tutayaafanya kazi na kuyachakata kuona tunaendaje katika suala zima la kuhakikisha sheria na kanuni zote zilizopo zilizopitwa na wakati ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hatua tuliyonayo. Lengo kubwa la Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona *NGOs* hizi zilizo ndani yetu zinapunguza utegemezi, zinakaa vizuri na kushiriki kuwa wanufaika wa Serikali yao kupitia *National Cake*. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kusisitiza juu ya kuuliza maswali kwa ufupi na Waheshimiwa Mawaziri kujibu kwa ufupi ili tutoe fursa kwa walio wengi zaidi.

Nimekuona Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. kwa kunipa nafasi. Pamoja na maelezo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mazuri ya Mheshimiwa Waziri, moja ya changamoto kubwa anayoanza nayo kwenye Wizara hii ni mauaji ambayo yanaendelea katika jamii hasa katika yanayosababishwa na jinsia, ikiwepo wanawake kuwaua wanaume, wanaume kuwaua wanawake, watoto kuwaua wazazi wao kwa ajili ya kupata mali:-

Je, Wizara imejipangaje sasa kabla ya kufikia kwenye vyombo vya usalama kuhakikisha kwamba wanazuia hali hii inayoendelea katika jamii?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE

NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kuhusu vitendo vya ukatili vinavyoendelea kwenye jamii yetu. Ni kwamba tunao mkakati wa kuto komeza ukatili kwa wanawake na watoto mpango wa Taifa uliozinduliwa mwaka 2017/2018 na unakwenda mpaka mwaka 2021/2022, ambao umeandaa Kamati kwenye ngazi ya Kijiji zinazoongozwa na Wenye viti wa Serikali za Kijiji, Mtaa, Kata, Halmashauri mpaka Taifa na mkoa ukiwemo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hizi tumeshazipelekea maelekezo na leo tunakwenda kuazimisha Siku ya Kupinga Ukeketaji tarehe 6 Februari, 2022. Hii ni Fursa ya kuziamsha hizi Kamati zote zifanye kazi yake. Zikitekeleza majukumu yake yaliyomo kwenye huo mwongozo, tutaweza kudhibiti ukatili huo unaotokea kwenye jamii kwa kuona viashiria husika na kuvitolea taarifa katika vyombo husika vinavyoshughulika na uhalifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eng Ullenge, nimkuona.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya swali la nyongeza. Licha ya Serikali kuleta Wizara hii maalum kabisa ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba kufahamu ni nini mpango wa Serikali kuajiri Afisa Maendeleo Jamii Kata

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na Afisa Maendeleo Jamii wa Vijiji ambao ni wachache sana ili wanawake wetu waweze kufikiwa na kuweza kukua kiuchumi? (*Makof*)

MWENYEKITI: Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Ulenge. Serikali inatambua upungufu wa watumishi hawa, Maafisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii. Kadri ya asilimia 96 kwenye Kata zetu hazina hawa watu; na kwenye bajeti ya mwaka huu tutapanga kuanza kupunguza upungufu huo kwa kushirikiana na wadau wetu.

MWENYEKITI: Tunakwenda Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, aulize swali lake.

Na. 20

Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mang'onyi

MHE. MIRAJI J. MTATURU Aliuliza:-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Mang'onyi ili kuongeza tija ya kilimo cha mbogamboga kwenye Kata za Mang'onyi na Makiungu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Wakili Msomi Anthony Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, napenda nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliye niwezesha kufika siku ya leo na kwa Ukuu wake. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu na kuahidi kwamba nitailinda imani hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Mang'onyi ambayo ipo Mkoani Singida imeendelezwa kwa kujengewa banio linalopokea maji kutoka Bwawa la Mwiyanji na takribani hekta 50 katika hekta 450 zimeendelezwa kwa kujengewa miundombinu ya umwagiliaji na sehemu ya shamba lililobaki hufikiwa na maji kwa njia ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Mang'onyi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mafupi kabisa. Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swalii la nyongeza.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mafupi ambayo bado hayajaondoa kabisa hamu ya wananchi wa Singida Mashariki kutumia banio hili. Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji kimeonekana ni kilimo chenye tija na hapa Bungeni tumekuwa tukizungumza mara kwa mara; na kwa kuwa soko la mbogamboga lipo kubwa sana kwenye mgodi wa *Shanta Gold Mine* pale Mang'onyi ambapo tunategemea utaanza hivi karibuni, ambalo litakuwa ni soko kubwa la mbogamboga na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali haioni umuhimu wa sasa kutenga fedha ambazo zilikadiriwa shilingi milioni 580 ili kuweza kukamilisha upande uliobakia kumalizia banio hilo lililokuwa limeandaliwa? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa chanzo cha maji na Bwawa la Mwianji alilolieleza limejaa tope na kusababisha maji kuwa siyo ya kutosha; na kwa kuwa tumekuwa tukipiga kelele kuhusiana na mabwawa hapa nchini yajengwe mengi ili kuongeza uwezo: Ni lini sasa Serikali itaweza kutenga fedha kwa ajili ya kuondoa tope za bwawa hilo la Mwianji ili liwe na kina cha kutosha na maji mengi na kuweza kujenga bwawa lingine ambalo litajengwa katika Kijiji husika cha Mang'onyi? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaruru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza na la msingi ni kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji. Kwa kuwa kilimo hiki kinagusa pia sekta ndogo ya mbogamboga, Serikali itaendelea kuweka mkazo mkubwa kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa hekta zilizobaki ili wananchi wa eneo la Mang'onyi waweze kupata huduma hii ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika ni kwamba, katika bajeti inayokuja tutatenga fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huu ili wananchi waweze kulima kuititia kilimo cha umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ili mradi huu uweze kutekelezeka vizuri, na Mheshimiwa Mbunge bahati nzuri amelieleza jambo hili vizuri na amekuwa mtetezi wa kweli kwa wananchi katika jambo hili, lazima katika fedha ambazo zitatengwa zijumuishie pia namna ya kuweza kuondoa tope katika Bwawa la Mwianji ili maji yaweze kutiririka kwa urahisi ili wananchi waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuondoe hofu; pia mimi na wewe tumepanga kwamba baada ya hapa tutakwenda kutembelea na

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuzungumza na wakulima ili kuona skimu nzima na kuona namna Serikali inaweza ikawasaidia kwenye skimu hiyi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Husna Sekiboko Mbwambo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Tanga, nimekuona.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ni maarufu sana kwa kilimo cha mbogamboga na matunda, lakini kilimo hicho kimeendelea kusuasua kutokana na kilimo hicho kutegemea zaidi mvua za asili:

Je, ni lini sasa Serikali itaandaa mpango wa kuvuna maji ya mvua ili baadaye yaweze kutumika katika umwagilia kipindi hicho cha ukame?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba ili kilimo chetu kiweze kuendelea, hatupaswi kuendelea tena kutegemea maji ya mvua. Kwa hiyo, kilimo cha umwagiliaji ndiyo tiba na ndiyo mwarobaini wa changamoto tuliyonayo. Kwa wakulima wa Lushoto, kazi inayofanyika pale kubwa ni lazima kuwajengea uwezo kwa kuhakikisha kwamba wanapata skimu hizo za umwagilaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo pamoja na Waziri wa Fedha wiki mbili zilizopita walifanya mkutano pamoja na Benki ya *BADEA* kwa ajili ya kupata mkopo wa kuja kujenga skimu kubwa za umwagiliaji ambazo zitasaidia sana kutatua changamoto katika maeneo mengi ndani ya nchi hii. Hivyo Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuiunga mkono Wizara yetu katika hatua ambayo tumefikia, basi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

fedha hizo za *BADEA* zikipatikana tuweze kujenga miradi mingi na mikubwa katika nchi yetu ili kilimo cha umwagiliaji kiweze kupata nafasi yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso, nimekuona.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Zipo skimu zilizoanzishwa na Serikali ikiwemo skimu ya Karema ambayo ilianzishwa toka miaka iliyopita kama saba hivi. Skimu hiyo haijafanya kazi na zipo nyingi nchini zinazofanana na ile skimu:-

Je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha miradi ilioanzishwa huko nyuma ukiwemo mradi wa skimu ya Karema?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo ameshatoa maelekezo kwa Tume ya Umwagiliaji Nchini kwa kuhakikisha ina *take stock* ya *scheme* zote nchini kwa zile zinazofanya kazi na ambazo zinahitaji ukarabati na zile ambazo zinahitajika kujengwa mpya. Hivi sasa kazi hiyo inaendelea na katika maeneo hayo pia tutaigusa skimu hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ya Karema; na tutatoa pia maelezo ndani ya Bunge letu hatua ambazo tumezifikia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii mikubwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Hai kwa asilimia 78 tunategemea kilimo cha umwagiliaji, lakini pia tunazo skimu 25 za kimkakati ambazo tukizitumia tutabadiishi kabisa maisha ya watu na sisi kushiriki katika pato la Taifa. Tarehe 21Januari, 2022 Mheshimiwa Rais akiwa anaelekeea Moshi Mjini alisimama pale Bomang'ombe, nami nilipata nafasi ya kumwomba atujengee skimu hizi. Alituahidi atatujengea kwa kutambua umuhimu mkubwa wa skimu hizi.

Swali langu, ni lini sasa Serikali itatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafue, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Rais ni maeleko kwetu na tumeipokea na tutaitekeleza kwa kadri ambavyo fedha zitaruhusu, kuanzia mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea ahadi ya Mheshimiwa Rais na tutaitekeleza kadri ambavyo fedha zitakuwa zinapatikana ndani ya Wizara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama nchi, ni muhimu kuwa na zao la kimkakati ambalo tuna uhakika wa kutupatia fedha za kigeni. Sasa kwenye zao la mbogamboga, *horticulture* hususan parachichi, sasa hivi kila mtu anajua kwamba kuna *demand* kubwa sana ya parachichi duniani na tafiti zilizofanyika karibuni, zinaonesha kwamba Tanzania ni kati ya nchi ambazo zinatoa parachichi bora kabisa duniani. Sasa kuna mikoa ambayo inalima parachichi, lakini ina mabonde ya asili yenye maji; ukzungumzia Njombe, Mbeya, Iringa, baadhi ya maeneo ya Songea na Songwe.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa Serikali, kwa kuzingatia maeneo haya yana mabonde ya asili, maji yanapatikana kiurahisi sana; kwa nini kusiwe na mkakati mahsus, ukizingatia *demand* kubwa ya parachichi duniani, haya mabonde yakaendelezwa kwa gharama nafuu, wananchi wakapata maji, kwa sababu parachichi ili liwe bora linahitaji maji na mbolea ili wananchi wapate na Serikali ipate: Sasa nataka majibu, katika hiyo mikopo ambayo mnasema mnazungumza, kuna mikakati gani mahususi ya kuendeleza mikoa hii mitano ili wakulima wanufaikie na Serikali inufaikie? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ndogo ya mazao ya mbogamboga na bustani, moja kati ya zao ambalo tumelipa kipaumbele kama Wizara hivi sasa ni zao la parachichi, kwa sababu tunatambua ya kwamba hivi sasa soko lake ni kubwa. Pia tumeshafungua masoko ya parachichi katika nchi za India pamoja na Afrika ya Kusini huku mawasiliano na majadiliano yakiendelea katika nchi za China na Marekani. Kwa kutambua umuhimu huo, katika mkopo huu ambao nimeuzungumza, moja kati ya maeneo ambayo yatakwenda kuguswa pia ni maeneo ambayo yanagusa mikoa hii ili kuhakikisha ya kwamba zao hili linapata huduma stahiki kutokana na upatikanaji wa maji mengi ya kutosha na pembejeo ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu kubwa katika hili ni kuifanya Tanzania ijulikane kwa parachichi kama zao la kipaumbele. Hatua ambazo zimeshachukuliwa kwa hivi sasa ni kwamba Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo ya ujenzi wa *common use facility* katikati ya mikoa ya Mbeya na Iringa ambayo itasaidia kulima parachichi yetu kwa ufasaha. Vile vile parachichi itakayovunwa itapelekwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwenye park moja ambayo tutafanya *sorting, grading* na *packaging* na kuifanya parachichi yetu ni *produce of* Tanzania kuliko hivi sasa ambapo parachichi yetu katika baadhi ya maeneo inaonekana kama inatoka nje ya nchi ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni hatua kubwa ambayo tumeichukua katika hatua ya awali kabisa, lakini lengo letu kubwa kabisa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kufungua masoko ya parachini lakini vilevile kuwajenglea wakulima uwezo na kulipa kipaumbele zao la parachichi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwenye zao la parachichi ambalo ni moja kati ya mazao ya kimkakati.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 21

Kampeni ya Kufanya Kilimo Biashara

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Je, ni Mikoa ipi inaongoza kwa mafanikio katika kampeni ya kuwabadiili wakulima kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kulima kibiashara na ni mikoa ipi bado inasuasua?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, karibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni ya kilimo biashara hapa nchini ilianza katika mazao yenye asili ya biashara ambayo ni pamoja na pamba, korosho, kahawa, pareto, chai, tumbaku na mkonge ambapo uhamasishaji wake ulifanyika kwa kuanzisha Vyama Vikuu vya Msingi vya Ushirika na Masoko (*AMCOS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa inayolima mazao ya kibiashara ni pamoja na Mwanza, Kagera, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara, Tabora, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Mtwara, Lindi na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Arusha, Ruvuma, Mbeya, Songwe, na Iringa. Kufuatia kazi kubwa iliyoofanya na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utoaji wa elimu ya kilimo biashara na utafutaji wa masoko ya mazao, wakulima katika mikoa hii wamebadilika na kwa sasa wanalima kilimo cha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa ambayo ilikuwa nyuma katika kutekeleza dhana ya kilimo biashara ilikuwa ni pamoja na mikoa ya Rukwa, Katavi, Kigoma, Dodoma, Singida, Morogoro, Manyara na Njombe. Mazao makuu katika mikoa hii ni yale ya nafaka, mikunde na mazao ya mafuta ambayo yalikuwa yakilimwa zaidi kwa ajili ya usalama wa chakula. Hivyo, kutokana na elimu ya kilimo biashara ambayo imekuwa ikitolewa kwa Maafisa Kilimo na wakulima katika mikoa hii, wakulima wengi wamebadilika na wanalima mazao kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jina langu ni Shally Josepha Raymond. Namshukuru Mungu sana kwa nafasi hii ya kupatiwa majibu haya mazuri na Serikali na nikuombe sasa niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amenieleza wazi, kuwa sasa hivi wakulima wanalima kutokana na wao wenyelewe

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

walivyoamua. Maamuzi hayo ni mazuri sana, lakini swalilangu la kwanza la msingi; kwa kuwa Serikali imeamua sasa kila mazao yanayolimwa yawe zaidi kibashara na nchi hii utakuta kwamba shida kubwa ni mbegu. Wakulima wako tayari kulima sasa hasa mazao ya mbogamboga na TAHA iko kazini masaa 24 kutoa msaada kwa wakulima wa mbogamboga. Je, Serikali iko tayari sasa kutoa ruzuku kwa mazao hayo yakiwemo maparachichi, alizeti, mbogamboga zozote ambazo zinalimwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalilangu la pili, wanawake wa Kilimanjaro wako tayari kulima kwenye vihamba vyao na Taasisi za Kilimanjaro za elimu, yakiwemo mashule yana mashamba ambayo yanayolimwa mara moja tu mahindi lakini mwaka wote mzima yanakuwa hayana kitu. Je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia wakulima hao na wakina mama wa Kilimanjaro, kulla maparachichi kwa wingi na Taasisi hizo kuchimbiwa mabwawa ili mashamba yale yasikae *idle* mwaka mzima? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza la kuhusu mbegu na ruzuku, ushauri huo tumeupokea tutakwenda kuufanya kazi. Isipokuwa tu nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeendelea kukiimarisha Kituo chetu cha Utafiti wa Kilimo kwa maana ya (*TARI*). Hata ukiangalia bajeti imeendelea kuongezeka kwa sababu tunataka tufanye utafiti wa mbegu bora na zenye tija, ili mkulima wa Tanzania anufaike na kilimo kiwe cha tija.

Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba eneo hili pia tumelipa kipaumbele na tunaendelea kuhakikisha kwamba, *TAR/inajengewa* uwezo ili kuja basi na tafiti ambazo zitatusaidia katika kilimo bora.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la kuwasaidia katika eneo la maparachichi hasa katika Taasisi zenyé mashamba ambayo hayatumiki muda wote. Kama nilivyosema dhamira ya Serikali katika sekta ndogo hii ya kilimo cha mazao ya bustani na mbogamboga ni kuhakikisha tunaipeleka mbele parachichi. Kwanza kwenye kuongeza uzalishaji wetu kwa sababu hivi sasa kama nchi tunazalisha tani 48,000 kwa mwaka. Lakini lengo letu ni kwamba ifikapo mwaka, 2025 tufikishe tani 140,000 ya parachichi na tuongeze pia *ku-export* parachichi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili hayo yote yaweze kutokea lazima tuweke mkazo mkubwa kuhakikisha kwamba tunasaidia kilimo hiki kukua. Hivyo, kwa wanawake wa Kilimanjaro ambao Mheshimiwa Mbunge amewaulizia swali hili, nataka tu nimwahidi ya kwamba, mimi niko tayari kuandaa ziara maalum katika maeneo yote ambayo umeyataja, tuyapitie kwa pamoja na vile vile tuimarishe vituo vyetu ili mpate miche ya kutosha, basi waweze kulima parachichi kwa sababu soko limeshakuwa kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza ambalo limejikita kwenye sekta hii hii ya zao la parachichi.

Nilisimama Bungeni hapa nikaomba kuhusu ugawaji wa miche ya parachichi kwa wakulima wetu. Kwa sababu, wakulima wetu wa Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Iringa wamejiwekeza sana kwenye kilimo cha parachichi, tukasema, kama ambavyo Serikali imefanya kugawa miche bure ya michikichi, miche bure ya pamba, miche bure ya korosho ili *ku-boost* wakulima wa mazao hayo, nikaiomba Serikali kuona ni mkakati upi ufanyike kwenye zao la parachichi ambapo wakulima wengi hawana fedha za

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kununua miche, lakini ni zao linaloonekana ni dhahabu ambalo sisi tunaita dhahabu ya kijani Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, Serikali ina mkakati upi wa kuandaa vitalu ili iweze kugawa miche bure kwa wakulima *ku-boost* zao hili, kutoka kwenye kilimo cha kawaida kwenda kwenye zao la biashara ambalo kwa sasa ni *hot* kwenye Taifa letu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nimekuona Hussein Bashe.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyojatoa ya ufasaha. Nataka nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imetoa ruzuku katika miche ya kahawa, tumetoa ruzuku katika miche ya korosho. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Serikali inafanya *mapping* katika mikoa mitano, inayozalisha parachichi na kwa kutumia Taasisi zetu za *TARI* na *TOSCI*, tumeanza kutengeneza *Regulation* na *Standardization* ili kuondoa tatizo la miche inayouzwa na kila mwananchi barabarani ili tusije tukaua zao la parachichi na hivi karibuni *tuta-launch* hizo *guideline*. Tunaanza programu kupitia *private sector partnership* kama Serikali kuanzia mwaka ujao wa fedha. Tutazalisha miche, tutagawa kwa *subsidized rate* kwa sababu sasa hivi najua wakulima wanununa katи ya shilingi 5,000 na shilingi 6,000 kwa mche mmoja ambao ni ghali sana. Kwa hiyo, tutaanza kugawa miche ya ruzuku ya parachichi katika mikoa yote inayolima parachichi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili tutakalofanya kama Serikali katika eneo la parachichi ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tutajenga *common use facility* tatu, moja tutaiweka katи ya lringa na Njombe nyingine tutaiweka Dar es Salaam na nyingine tutaiweka Mkoa wa Kilimanjaro. Hizi zitatumika, wale wanunuzi wanaotoka nje

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

watanunua parachichi, watafika katika hizo *facility*, watapata huduma kwa kuzilipia na zitawekwa alama ya kwamba ni *product* za Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji. Timu yetu ya Umwagiliaji sasa hivi inafanya *mapping* katika mikoa hiyo ili tuone ni wapi ambapo tutaweza *ku-facilitate* kuweza kugawa mipira na nini ambako wananchi wamewekeza. Kwa sababu ni zao ambalo linahitaji uwekezaji wa muda mrefu na linahitaji *government intervention*, ni wahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge tutafanya *strong intervention* kwenye parachichi kwa sababu tunaamini tunazo *competitive aids* zote. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Humphrey Polepole.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tanzania ni mojawapo ya nchi mbili Ulimwenguni ambazo zimepewa baraka na Mungu ya kuzalisha *organic phosphate*. *Organic phosphate* ni mojawapo ya madini muhimu yanayotumika kutengeneza mbolea. *Organic phosphate* ulimwenguni inapatikana Tanzania na Australia peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia *ku-export organic phosphate* kama ambavyo inaendelea kufanyika sasa hivi, ili ibaki hapa nchini na kuendelea kuzalisha mbolea ili wakulima wetu wapate mbolea hapa na pasipo na kuhangainika kutoka maeneo mengine? Natambua kiwanda kinakuja Dodoma lakini kuna tamaa kubwa sana ya *ku-export organic phosphate* kwa sababu ni nchi mbili tu ulimwenguni ambazo zinatoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Polepole, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nchi tunakuwa guided na *WTO Regulation za Trade*. Kwa hiyo, *ku-declare openly* tunazuia *export* au biashara yoyote sidhani kama katika misingi ya kibiashara ni jambo jema. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili sisi kama Serikali tumeshafanya *comprehensive analysis* kuangalia *deposit* yetu ya *phosphate* iliyopo katika nchi yetu. Tunazo taratibu za kuruhusu mahitaji yanapohitajika kwenda nje tunazo *guidance zinazotu-guide*. Haturuhusu *exportya* holela katika *phosphate*. Hilo la pili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu kwa kuwa tumeshapata Mwekezaji ambaye anawekeza na atatumia *phosphate* katika Kiwanda cha Mbolea, kinachojengwa hapa Dodoma ambacho kinazalisha tani 600,000 na kitaanza mwaka kesho mwezi wa pili kuanza kuzalisha. Nataka niwahakikishie tu wakulima kwamba tuta-regulate matumizi ya rasilimali hii kwa maslahi ya Watanzania bila kuathiri mahusiano yetu ya kibiashara na nchi zingine. (*Makof*)

MWENYEKITI: Sasa tunakwenda Wizara ya Maji, namwita Mheshimiwa Condester Sichalwe aulize swali lake.

Na. 22

Changamoto ya Maji – Mombasa

MHE. CONDESTER M. SICHALWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji katika Jimbo la Mombasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Mombasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosha. Upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Mombasa ni wastani wa asilimia 59.07 kuititia visima vifupi (16), visima virefu (43), skimu za usambazaji maji (17) na matanki ya kuvunia maji ya mvua (3). Katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Mombasa, Serikali inatekeleza miradi ya maji katika Vijiji 13 vya Nkangamo, Itelefya, Mbao, Mkonga, Papa, Masanyinta, Kasamu, Samang'ombe, Lwatwe, Ivuma, Kapele, Mkutano na Kalungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matanki saba (7) yenye ujumla ya ujazo wa lita 600,000, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 32, vituo vya kuchotea maji 66 na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 72. Utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani wa asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha upatikanaji wa huduma ya maji. Serikali itaendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi mwaka hadi mwaka ili kumaliza tatizo la maji katika Jimbo la Mombasa na kufikia lengo la asilimia 85 ifikapo mwaka, 2025.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sichalwe, swali la nyongeza.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado, changamoto ya maji kwenye Jimbo la Mombasa ni kubwa sana. Naomba kuiuliza Serikali niongeze maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji ambavyo umevieleza tunavyo vijiji 72 na vitongoji 302 inaonyesha

kwamba hata nusu ya vijiji hivyo vitakuwa bado havijapata maji safi na salama. Ombi langu kwa Serikali, viko baadhi ya visima ambavyo vilishawahi kuchimbwa nyuma na wakoloni, vilishawahi kuchimbwa nyuma na wamisionari lakini pia na baadhi ya wakandarasi ambao walikuja kujenga barabara kwenye Jimbo la Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, nini kauli ya Serikali kwenda kuvitembelea visima vile ambavyo vimeshawahi kufanya kazi vizuri huko nyuma kutokana bado kuna changamoto ya maji vinaweza vikatusaidia vikawa kama njia nyingine ya mbadala kutatua changamoto ya maji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa, baadhi ya vijiji ambavyo vimeonyesha vinao miradi hiyo ya maji lakini zipo Taasisi kama Vituo vya Afya, Zahanati pamoja na Sekondari havipati utoshelevu wa maji. Watoto wetu especially wa kike wameendelea kuteseka sana kufuata maji wakati mwingine zaidi ya kilomita 10. Mfano, Shule ya Sekondari Chikanamlilo, Shule ya Sekondari Mombasa, Shule ya Sekondari Uwanda, Shule ya Sekondari Ivuna, Shule ya Sekondari Nzoka na shule zingine 13 ambazo ziko ndani ya Jimbo la Mombasa pamoja na Zahanati na Vituo vya Afya kama Kamsamba na Kapele. Je, ni nini kauli ya Serikali kutuchimbia visima virefu ili Taasisi hizi ziweze kujipatia maji yake bila kutegemea kwenye vile vituo ambavyo tunang'ang'anira na wananchi na havitoshelez? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kutembelea visima ambavyo ni chakavu hii ni moja ya jukumu letu na tayari, Mheshimiwa Waziri amewaaagiza watendaji wote kwenye mikoa yote, kwa maana ya *Regional Managers (RMs)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na *Managing Directors (MDs)* wasimamie visima vyote ambavyo ni chakavu. Vile ambavyo uwezekano wa kuvirejesha katika hali njema ya kutoa maji safi na salama vyote viweze kurejeshwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Jimbo la Mombasa sisi kama Wizara tumeshaleta Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuchimba visima virefu. Hivyo, visima hivi ambavyo vyatukarabati lakini uchimbaji wa visima virefu kwenye swali lako la pili la nyongeza, navyo tayari vimeshaanza kufanyiwa kazi katika baadhi ya maeneo. Tayari visima vitano vimeshachimbwa kati ya visima 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, napenda tu kumtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba sisi kama Wizara tutakwenda kuhakikisha katika sehemu zote ambako Taasisi za Serikali zipo kama zile Shule alizozitaja pamoja na Vituo vyta Afya na Hospitali maji ni lazima yafike na huo ndio *Motto* wa Wizara. (*Makofisi*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Cecil Mwambe Mbunge wa Ndanda, uliza swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye Jimbo la Ndanda tuna mradi mkubwa wa maji uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni tano uliokusudiwa kuhudumia Kata ya Mwena, Kata ya Chikundi pamoja na Kata ya Chikukwe. Hata hivyo mradi huu unafanya kazi kwa kiwango cha chini kabisa kwa sababu inaonekana ili kuwa ni *poor designing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, je, haoni haja ya kuwaagiza wataalam wake wakakague mradi huu na kupeleka mapendekezo bora Serikalini, ili kuweza kuboresha ili wananchi wa Kata hizo wapate maji kwa kipindi chote cha mwaka?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la kupeleka wataalam wakakague mradi huu na ni mradi ambao unakwenda kugharimu Serikali fedha nyingi zaidi ya Shilingi bilioni tano. Hii ni moja ya majukumu yetu Mheshimiwa Mbunge, tayari Mheshimiwa Waziri, amewasisitiza sana watendaji wanatakiwa kufuatilia hii miradi. Hivyo, nami napenda kusisitiza *Managing Director* na *Regional Manager* wa Mkoa wa Mtwara wahakikishe wanakwenda kusimamia huu mradi kuona unatekelezwa kadri ambavyo unapaswa kuwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Changamoto ya maji iliyopo katika Jimbo la Mombasa haitofautiani na changamoto iliyopo katika Jiji la Dodoma, kwamba kuna baadhi ya maeneo yamekuwa yakikosa maji hata kwa wiki tatu kwa maelezo kwamba mitambo ya Mzakwe imezimwa kutokana na ukosefu wa umeme.

Napenda kufahamu, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na kadhia hii ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kukosa maji mara kwa mara. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Maji.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Naibu wangu kwa kazi nzuri na namna gani anavyojibu maswali hapa Bungeni. Hata hivyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge, lakini kwanza nimpongeze Mama yangu Toufiq, kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika Mkoa huu wa Dodoma. Tukiri kabisa sisi kama Wizara ya Maji hapa Jiji la Dodoma kumekuwa na ongezeko kubwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

la watu, uhitaji na uzalishaji wa maji katika Jiji la Dodoma uwezo wa mtambo wetu ni lita milioni 60 na mahitaji yake ni lita milioni 103 kutokana na ongezeko kubwa la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo maelekezo mahususi ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa Wizara yetu ya Maji, kwa sababu lazima tumtue mwana mama ndoo kichwani. Tunakwenda kuyatoa maji ya Ziwa Victoria na kuja kuyaleta katika Jiji hili la Dodoma, ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na changamoto hii. Kwa mkakati wa muda mfupi tunaendelea kuchimba visima virefu katika maeneo mbalimbali, ili kuongeza uzalishaji kwa muda mfupi na wananchi waendelee kupata huduma ya maji. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAI FUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Jimbo la Tabora Mjini ni katи ya Majimbo ambayo yamenufaika na Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, lakini mpaka sasa baadhi ya maeneo ya Jimbo hilo hayana maji kabisa. Je, Serikali imekwama wapi kusambaza maji kwa wananchi wa Tabora Mjini? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa, kutoka Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule mkubwa kutoka Ziwa Victoria ni mradi ambao ni endelevu na ni mradi wenye manufaa makubwa sana. Maeneo mengi ambayo yamekuwa yanapaswa kupitiwa na mradi ule yataendelea kupata maji kwa wakati wote. Kwa maeneo machache ambayo kama bado hayajapata maji, wataalam wetu wanaendelea kufanya kazi kuhakikisha usambazaji wa maji ni zoezi endelevu. Hivyo waendelee kuvuta subira muda si mrefu na wao watapata maji. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge Viti Maalum kutoka Songwe.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza. Ni wazi Wizara hii imekuwa ikifanya kazi kubwa kuhakikisha huduma ya maji inafika katika maeneo mengi. Katika maeneo ya Majiji, Manispaa na Miji kumekuwa na changamoto ya milipuko ya moto. Ambapo ukiuliza unaambiwa visima vya maji ambavyo vitajaza kwenye magari maji kwa wepesi havipo. Swali langu nilitamani kufahamu ni nini mkakati wa Wizara kuhakikisha katika *project*, kila mradi unaokuwa unaandaliwa kunakuwa na *setting* ya visima au matanki ambayo yatajaza maji kwa haraka katika magari ya zimamoto? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila, kutoka Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swali aliloliuliza ni utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani na hawa wenzetu wa Zimamoto wanaufahamu wajibu wao. Taasisi zote za Serikali ambazo zinahitaji huduma ya maji wanafahamu wanapaswa kufika katika ofisi zetu kwenye mikoa yao. Ili waweze kuongea na wataalam wetu na kuona njia njema ya kutumia ili waweze kupata huduma ya maji katika ofisi zao. Taasisi zote za Umma zinapeleka maji kwa gharama zao na pale inapobidi kupata huduma ya kiupendeleo basi huwa wanafika na kuweza kueleza tatizo husika. Hivyo, wenzetu wa Zimamoto wanafahamu wapi wafike ili waweze kufanya vyema. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Maji. Sasa namwita Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 23

Hitaji la Majisafi Wilaya ya Kyerwa

MHE. ANATROPIA L. THEONEST aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia maji wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kwa kutengeneza miundombinu ya kupeleka maji kwa Wakazi waishio sehemu za miinuko.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Wilayani Kyerwa ni wastani wa asilimia 56.8. Katika kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na wale wanaoishi kwenye maeneo yenye miinuko, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mipy ya Kagenyi - Omukalinzi na Mabila. Ujenzi wa miradi hiyo unahusisha ulazaji wa bomba umbali wa Kilometra 7.2, matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 105,000 na vituo sita vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hii umefikia asilimia 70 na umepangwa kukamilika mwichoni mwa mwezi Juni, 2022. Sambamba na miradi hiyo, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuajiri Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya Runyinya - Chanya, Kimuli - Rwanyango na Nyamiaga - Nyakatera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo, itahusisha ujenzi wa matenki matano yenye jumla ya ujazo wa lita 1,700,000, ulazaji wa mabomba umbali wa Kilometra 86.1 na ujenzi wa vituo 146 vya kuchotea maji. Kukamilika kwa miradi hiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kutanufaisha Vijiji vya Nkwenda, Runyinya, Rwabwere, Muhurire, Karongo, Iteera, Muleba, Chanya, Chakalisa, Kagu na Nyakatera. Vijiji vingine ni Chakalisa, Kishanda, Nyakahita, Kyerwa, Nyaruzumbura, Milambi na Katera. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imesaini mkataba mwezi Januari, 2022 na Mkandarasi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji Kijiji cha Murongo kwa kutumia fedha za UVIKO-19. Mradi huo unahusisha ujenzi wa tenki moja la lita 150,000, ulazaji wa mabomba umbali wa Kilometra 16.6, ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji. Mradi huo unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2022. Kukamilika kwa miradi yote hiyo kutaboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Wilaya ya Kyerwa. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ili kuhakkisha kuwa huduma ya maji safi na salama ndani ya Wilaya ya Kyerwa inafikia kiwango kisichopungua asilimia 85 mwaka 2025.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia, swalii la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa majibu yaliyotolewa, lakini watu wa Kyerwa hawana majikwa asilimia 56 kama Serikali inayoeleza. Changamoto ya upatikanaji wa maji ni kubwa zaidi, naweza kusema ni asilimia kama 25. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye mkakati wa maksudi wa kuwasaidia watu wa Kyerwa wapare maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu ni kwamba, ametaja Mradi wa Runyinya, Chanya, Kimuli, Rwanyango, Nyamiaga na Nyakatera ambapo ukiweza kusainiwa na kuanza utapunguza kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa maji. Nataka kujua ni lini sasa mkataba utasainiwa kwa sababu imekuwa ni kila siku mkataba unakaribia kusainiwa. Nataka nijue ni lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili. Wananchi wa Kata za Nyakatuntu, Kimuli, Kamuli, Bugara na maeneo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mengine wana changamoto kubwa ya maji na wameahidiwa watakuwa kwenye mradi wa vijiji 57 ambapo iwapo utatekelezwa ungepunguza changamoto ya maji. Haujaanza na hatujui unaanza lini. Nataka nijue ni lini huo mradi utaanza na kukamilika ili kuondoa adha kubwa ya maji kwa wananchi wa Jimbo la Kyerwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anatropia kwa maswali yake mazuri na ninamwona ana ushirikiano wa karibu sana na Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge mwenye Jimbo, ambaye ameendelea kufuatilia miradi hii yote. Mheshimiwa Innocent Bilakwate ni juzi ametoka Ofisiini kuhakikisha anaweka sawa miradi hii ambayo inaenda kufanyika katika Jimbo la Kyerwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna mradi wa Kamuli ambaao kijigrafia upo juu. Tunatarajia mradi huu kwenda kutekelezwa hivi karibuni na utekelezaji wa mradi huu utasaidia kusambaza maji katika vijiji vingi vya Jimbo la Kyerwa. Hivyo, napenda kukutoa hofu Mheshimiwa Mbunge, miradi hii itasainiwa kwa taratibu za Wizara zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *percentage* za usambazaji maji katika Jimbo la Kyerwa ni asilimia za kitaalam, siyo za kufikirika kuangalia tu kwa macho na ukasema ni asilimia 20. Ni asilimia zilizotajwa na watalaam, zimefanyiwa kazi na tuna uhakika na kazi tunayoifanya. Nasi Wizara ya Maji siyo wababaishaji, lengo letu kubwa ni kuhakikisha tunamtua ndoo mama kichwani kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu anatutaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika eneo hili. (*Makofi/Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aaah!

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Kimsingi makofi haya yanadhihirisha ulivyoeleweka na jinsi ambavyo unatambua kazi ya Mheshimiwa Mbunge, lakini zaidi ya Mheshimiwa Bilakwate. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea. Nimekuona Mheshimiwa Monni.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Changamoto iliyopo kwenye Jimbo la Kyerwa inafanana kabisa na changamoto zilizopo Wilaya ya Chemba. Changamoto kubwa ni miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwa kupitia Wizara ya Maji, nami ni shabiki mkubwa wa Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso. Yale maneno ambayo Ndugu yangu Mheshimiwa Jerry Silaa alisema, nami nayathibitisha kwamba anapaswa kupewa zile *Ph.Dambazo* zinatolewa, tena apewe Tanzania. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu sasa. Pamoja na kuwa tumepata visima vitano na vimechimbwa zaidi ya miaka miwili, vingine mmoja, lakini bado havifanyi kazi kwa sababu miundombinu yake haipo tayari:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, ni lini sasa Serikali kupitia Wizara ya Maji itaweka miundombinu ili watu wale nao waanze kupata maji? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi. Nimekuona Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Chemba kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa muda mfupi katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kweli tulishafika Chemba, hali ya Chemba ilikuwa siyo nzuri. Maelekezo ya kwanza ambayo tumeyafanya ni katika kuhakikisha kwamba

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tunachimba visima vya dharura ili wananchi wa Chemba waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Nataka nimhakikishie katika mfuko wa mwezi huu tutatoa fedha ya uanzaji wa miradi ile ili wananchi wa Chemba waweze kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumaliza kabisa tatizo la Maji Chemba, siyo maeneo yote ambayo utachimba ukapata huduma ya maji. Eneo la Chemba limetupa *experience baadhi ya maeneo yamekuwa na ukame.* Tunakwenda kuchimba bwawa kubwa katika kuhakikisha wananchi wa Chemba wanaendelea kunufaika na maji. Tunaona mvua zinazonyesha maji yanapotea tu. Mkakati wa Wizara na mageuzi ya Wizara ni kuhakikisha tunachimba mabwawa makubwa ili kuvuna maji na wananchi wa Chemba waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa. (*Makofii*)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nianze kwanza kwa kutoa pongeza nyingi sana kwa Serikali kwa namna ilivyoshughulikia matatizo ya wananchi wa Jimbo la Buchosa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa juhudii zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi wa Lumea, Nyakariro, Karebezo hadi Nyehunge wa shilingi bilioni 1.6. Mradi huu ni kichefuchefu, ulijengwa chini ya kiwango, mabomba yanapasuka, maji yanamwagika chini na wananchi hawapati maji:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini atatembelea mradi huu ili kuweza kuwa na utaratibu wa kufanya maboresho na wananchi waweze kupata maji?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Pili, ni lini Serikali itapeleka watalaan kuchunguza na kugundua watu waliohusika na ubadhirifu kwenye mradi huu ili waweze kuchukuliwa hatua kuepusha kuharibu sifa ya Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Eric Shigongo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kwenda kutembelea Mheshimiwa Mbunge mantahofu, mara baada ya Mkutano huu tutakwenda kutembelea na kujionea na kuona kwamba kazi zinaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Watalaan kwenda kuchunguza, Mheshimiwa Waziri ameshatengeneza *task force* ya kufuatilia miradi yote kichefuchefu na kuona kwamba inafanyiwa kazi na inakamilika na huduma ya maji inapatikana bombani na tunamtua ndoo mwanamke kichwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, napenda kusema kwamba, ile *task force* naamini wamesikia na ninasisitiza maagizo ya Mheshimiwa Waziri mara wasikiapo maagizo haya waweze kwenda mara moja ili kuchunguza na miradi ile iweze kukamilika na lengo la kutoa maji na kumtua mama ndoo kichwani liweze kutimilika. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Askofu Gwajima, swal la nyongeza.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swal moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Jimbo la Kyerwa la maji, linafanana sana na tatizo la Jimbo la Kawe; na kwa kuwa ndugu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

alikuwa na mradi unaotokea Ruvu Chini mahali ambapo amejenga matenki Mabwepande, Bunju A, Tegeta, Salasala na maeneo mengine ya Jimbo la Kawe; na mradi huu ulitegemewa mwisho wa mwaka Desemba uwe umeshakamilika ili watu wapate maji, lakini mpaka leo Madale, Nakasangwe, Kisauke, Mabwepande, Tegeta hazina maji:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa mradi huu utakamilika ili wananchi wangu wa Jimbo la Kawe wapate maji? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Mheshimiwa Waziri wa Maji nimekuona.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa kweli nilpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo la Kawe. Kwa kweli maeneo ya Mabwepande yamekuwa na changamoto kubwa sana na tunaona kazi kubwa inayofanywa na DAWASA. Naomba baada ya saa 7.00 tukutane, tufanye mawasiliano na Mkurugenzi wa DAWASA ili tuweze kutia nguvu kwa pamoja na mradi ule uweze kukamilika na wananchi wa Mabwepande waendelee kupata huduma ya maji. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naona mikono bado ni mingi na vi-memo zaidi ya kumi visto hapa, lakini muda haupo nasi.

Tunaenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, sasa namwita Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 24

Hitaji la Lughya ya Alama kwenye Mitaala

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu nchini?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu Swalil Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Lugha ya Alama katika kuondoa kikwazo cha mawasiliano kati ya wenyewe uziwi na wale wasio na uziwi. Katika kufikia lengo la kuingiza Lugha ya Alama kwenye Mitaala ya Elimu nchini, Serikali imekamilisha usanifishaji Kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania ya mwaka 2020 na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na mawasiliano. Vilevile, Serikali imekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuandaa walimu wenyewe taaluma ya Elimu Maalum katika fani ya Uziwi na Lugha ya Alama kila mwaka. Aidha, Serikali inaendelea kupokea maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu na mafunzo nchini ambapo suala la matumizi ya Lugha ya Alama katika mitaala hii litazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ikupa, swali la nyongeza.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza na kuishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo inazishughulikia changamoto mbalimbali za watu wenyewe ulemavu ikiwemo changamoto hii ya lugha ya alama; na ikikumbukwa kwamba changamoto hii niliweza kuizungumzia sana katika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Bunge la Kumi na Moja, lakini hatimaye leo hii Serikali ya Awamu ya Sita imeanza kulifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia jamii yetu, yaani tunandaa kizazi ambacho kitaweza kuwasiliana na viziwi kwa maana ya Polisi, Walimu, Madaktari hata kwenye familia zetu. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali. Sina uwezo wa kupiga magoti, ningepiga magoti kuishukuru Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza la nyongeza ni kwamba, ni lini sasa mchakato huu utakamilika na hatimaye mitaala hii kuanza kutumika ndani ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wakati tunasubiri ukamilishwaji wa mchakato huu, Serikali ina njia gani mbadala ya kuinua kiwango cha elimu kwa wenzetu vizili? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba tupokee hizo pongezi za Mheshimiwa Rais kwa niaba yake, lakini tunaamini pongezi hizi zimemfikia na hiyo ndiyo Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan na huo ndiyo wajibu wetu kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge Iako Tukufu kwamba mchakato huu wa maboresho ya mitaala yetu ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alioutoa tarehe 22 Aprili, 2021. Mara tu baada ya maagizo yale, sisi kama Wizara tulikaa na kuanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu huwa unachukua muda mrefu, ni kati ya miaka mitatu mpaka mitano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi kisichozidi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

miaka mitatu na miezi tisa mitaala yetu hii mipya iweze kuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako Tukufu, ifikapo mwaka 2025 Januari, mitaala yetu mipya itakuwa tayari kuanza kutumika katika maeneo yote kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili amezungumzia juu ya namna gani watoto wetu tunawachukuwa kwa sasa hivi? Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo mbioni na inaendelea kuwahudumia wanafunzi hawa au watoto wetu hawa. Kwanza tuna shule ya msingi ambazo tumejenga kule Mtwara inayoitwa Lukuledi kwa ajili ya kuwachukua wanafunzi hawa wenye matatizo ya uziwi kwa upande wa Shule za Msingi. Vilevile kule Patandi Arusha, tuna Shule ya Sekondari kwa ajilli ya wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kipindi hiki tumeweza kutoa mafunzo kwa Walimu kwenye shule ambazo zinachukua wanafunzi wenye uziwi katika shule zetu zote za Sekondari katika kipindi kilichopita; na pia mwezi Machi mwaka huu Walimu wetu wa Shule za Msingi kwa shule zinazochukua wanafunzi hawa, nao vilevile tutawapa mafunzo ya lugha ya alama na kuwapa mbinu za namna ya kuwafundisha wanafunzi hawa. Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa sana wa Walimu wa Elimu Maalum nchini Tanzania na hasa katika Mkoa wangu wa Songwe; na sasa hivi Serikali ina-*practice inclusive education* kwa maana ya elimu jumuishi:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka iwe ni *compulsory* kwa kila Mwalimu ambaye anasomea masuala ya elimu, kusomea elimu maalum kwa ajilli ya watoto wetu?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Shonza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi, amezungumzia suala la *inclusive education* na nimeeleza, katika kipindi kilichopita tumeweza kutoa mafunzo kwa Walimu wote wa Shule za Sekondari katika shule zile ambazo zinachukua wanafunzi hawa wenye uziwi. Katika mwaka huu tunatarajia mwezi Machi tutafanya mafunzo kwa Walimu wote wa shule za msingi zile ambazo zinachukua wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa vile lengo lake ni kuhakikisha kwamba mitaala yetu inakwenda kuboreshwa ili somo hili liwe *compulsory*, hili ni eneo ambalo tutakwenda kulifanya kazi katika uboreshaji wa mitaala hii ili wakati tunapoanda mitaala, masomo ya lugha ya alama na mbinu za kufundishia wanafunzi wenye uziwi yaweze kuingia kwenye mitaala yetu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge Viti Maalum, Arusha.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swalii dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwawezesha vijana wetu waweze kupambana na changamoto za uchumi wa kidigitali. Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza rasmi somo la TEHAMA, hususan kwa vitendo, katika mitaala yetu ya elimu ya msingi? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Juma Omar Kipanga.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi. Kwa vile tunaenda kuboresha mitaala yetu na anazungumzia suala la TEHAMA kuweza kuingia katika mitaala yetu ili liweze kuwa *compulsory*, huu ndio wakati muafaka. Tunaomba tuyabebe mawazo haya na kwa vile tunaenda kuboresha tunaamini kabisa mtaala tutakaokuja nao ni ule ambao utakwenda kukidhi mahitaji ya Waheshimiwa Wabunge, lakini na Waheshimiwa wananchi wa Tanzania. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Mjini, Mheshimiwa Zacharia P. Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Shule ya Msingi ya Endakoti katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ina wanafunzi 40 wa elimu maalum. Shule hiyo iliyojengwa mwaka 1929 inakabiliwa na changamoto ya miundombinu. Je, ni lini Serikali itatekeleza azma yake ya kuteua shule mojawapo kila halmashauri itakayochukua wanafunzi wa elimu maalum ili vitengo hivyo viboreshwe kupata miundombinu na huduma nydingine?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Zacharia kwa kuona umuhimu wa watoto wetu hawa kuweza kupata mazingira wezeshi na miundombinu wezeshi ili kuweza kufikia ndoto zao. Suala la uboreshaji wa mazingira ni suala endelevu na nadhani tumeona kwenye Serikali yetu kwenye kipindi hiki kifupi kilichopita zaidi ya trilioni

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

1.3 tulizopata zimeweza kwenda kwenye eneo kubwa sana la miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika kipindi kijacho, kwa vile sasa tunaandaa bajeti, tutahakikisha kwamba, maeneo haya ambayo yanachukua wanafunzi wetu wenyewe mahitaji maalum tutakwenda kuyafanya kazi na kuyapa kipaumbele kuhakikisha kwamba, yanapata miundombinu wezeshi, lakini vilevile na Walimu wa kutosha kwa ajili ya kuwafundisha watoto wetu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa namwita Mheshimiwa Daktari Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 25

Vijana Wote Kupata Mikopo ya Elimu ya Juu

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsus wa kuhakikisha vijana wote wanaoomba mikopo ya Elimu ya Juu wanapata mikopo hiyo kama walivyoomba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
aliibju:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kugharamia utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo iliyopo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila wanafunzi wa Elimu ya Juu mhitaji anapata mkopo kwa ajili ya kugharamia masomo yake. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imekua ikiongeza fedha za bajeti ya mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kila mwaka. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ikiwa ni ongezeko la bilioni 106 kutoka bilioni 464 ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko hilo la fedha za bajeti, wanufaika wa mikopo ya Elimu ya Juu wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka, ambapo katika mwaka 2021/2022 wanafunzi wanufaika wa mikopo ya Elimu ya Juu walikua 176,617 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 27,228 kutoka wanafunzi 149,389 wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza fedha za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kulingana na ongezeko la fedha katika bajeti yake ili kuhakikisha vijana wote wanaoomba mikopo ya Elimu ya Juu wanapata mikopo hiyo kama walivyoomba. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa, idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita inaongezeka mwaka hadi mwaka; na kwa kuwa, bajeti yetu na uwezo wetu wa kuwagharimia kupata mikopo sio mkubwa sana. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuanza maongezi na mazungumzo na benki za kibashara, ili Serikali iwadhamini vijana wetu ambao wanakosa mikopo, ili wapate mikopo kuititia benki za biashara kwa riba nafuu ambayo Serikali itaweza kuwadhamini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ametuletea pendekazo, ametuletea wazo. Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge naomba nilihakikishie Bunge lako tunaomba tulibebe pendekazo hili la Mheshimiwa Dkt. Kikoyo twende tukakae chini, tulifanyie kazi, tufanye tathmini ya kina na pindi tutakapoona kwamba, jambo hili linafaa, basi tutakuja kulieleza kwenye Bunge lako Tukufu ni namna gani ya kuliendea jambo hili. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa jibu zuri Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaamini mtaenda kufanya kazi, illi kuweza kusaidia vijana wengi wa Kitanzania ambao wana changamoto hiyo.

Nimekuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kiuhalisia Wizara ya Elimu ni miongoni mwa Wizara ambayo inaonekena inatengewa bajeti kubwa, lakini unakuta pesa nyingi katika Wizara hii ni pesa za mikopo ya elimu ya juu ambayo mara nyingi wanaziweka kama ni fedha za miradi ya maendeleo, lakini kimsingi pesa zile zilitakiwa ziwe kwenye matumizi ya kawaida kwa sababu, zinaenda kuwasaidia vijana wetu pesa za kujikimu. Hii imekuwa ni mapendekezo ya Kamati mbalimbali, ikiwepo Kamati ya Bajeti.

Je, illi kuitendea haki Wizara hii kwa nini hizi pesa za mikopo msiziweke kwenye matumizi ya kawaida ili sasa tujue, kama Bunge, tuna jukumu gani la kutenga pesa za kutosha kwenye miradi ya maendeleo iende kwenye utekelezaji? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hili ni wazo la Mheshimiwa Mbunge na amesema kwamba, ni mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati mbalimbali, sisi kama Wizara tutaenda kukaa na Wizara ya Fedha kuweza kuona namna gani jambo hili linaweza kwenda kufanyiwa kazi, lakini kimsingi tunaomba tulibebe. Ahsante.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbunge wa Sikonge.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa mitaala pamoja na mikopo huzalisha wahitimu na kwa sababu, Wizara hii ndio Wizara ya kisera. Kwa mujibu wa taarifa ambayo ilitolewa hapa Bungeni na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mwaka, kati ya ajira zilizombwa za ualimu elfu 10, walioajiriwa kama elfu 10, lakini waombaji walikuwa zaidi ya laki moja. Maana yake ni kwamba, ukiangalia mpaka waliohitimu mwaka jana ukijumlisha pale ni zaidi ya laki moja wako mtaani hawajapata ajira. Sasa swali langu, ni kwa nini Serikali au Wizara hii wasijadili hili suala la ajira ili kuwasaidia, hasa Walimu ambao ni Walimu wa Kiswahili, waende kufundisha Kiswahili kwenye nchi za Afrika Mashariki pamoja na *SADC*?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Omar Kipanga.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swalii dogo la Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira ni suala ambalo ni mtambuka na kwa vile Mheshimiwa Mbunge anatoa pendektezo kwamba, tuweze kuangalia namna gani tunaweza tukawasaidia Walimu kwenda kufundisha kwenye

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

nchi hizi za Afrika Mashariki na Kati na Kusini mwa Afrika, tunaomba vilevile suala hili tulichukue, twende tukaangalie hizo fursa ambazo zinatokea kwenye nchi hizo na namna gani tunaweza tukakaa kitako na kuweza kushawishi namna gani Walimu wetu ambao wamehitimu kwenye shahada mbalimbali za ualimu, hasa hizi za Kiswahili kwenye vyuo vyetu, wanaweza kwenda kutumika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunajua kwamba, masuala ya ajira mara nyingi sana *yanocompetition* zake kwa sababu itakwenda kwenye usaili na watahitajika kwenda kwa ajili ya usaili huo. Kwa hiyo, hatuwezi kutoa *guarantee* moja kwa moja kwamba, tutafanya hivyo kwa asilimia 100, lakini nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunalichukua, tutaenda kulifanyia kazi na kuweza kuangalia namna gani nafasi hizo zinapatikana na tunaweza kunufaika sisi kama nchi.

MWENYEKITI: Wauliza maswali bado wako wengi. Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo, Mheshimiwa Justin.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika uendelezaji wa sekta ya afya pamoja na sekta nyingine kuna watumishi ambao wanahitajika sana sasa hivi, kwa mfano *clinical officers*, wafamasia na hawa hawasomi vyuo vikuu. Kumekuwa na pendeleko la muda mrefu sana la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati ambalo ni hitajti kubwa sana katika nchi yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati pia wanapata mikopo kwa sababu, ndio mahitaji makubwa katika nchi yetu kulingana na miundombinu tunayojenga kwenye maeneo ya vijiji ambayo yanahitaji sana hiyo kada ya kati kulitumikia Taifa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swalidogo la nyongeza la Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli analozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba, uhitaji uko mkubwa sana kwenye vyuo vyetu nya katilakini kama tunavyofahamu na kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swalila msingi, jambokubwa hapa ni suala la bajeti. Iwapo kama bajeti yetu inaruhusu tunaweza tukavifika vyuo vikuu vyote, lakini vilevile pamoja na vyuo nya katil. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, bajeti itakaporuhusu tutahakikisha tume-coverkwanza eneo lote la vyuo vikuu halafu tutaangalia namna gani sasa mikopo hii inaweza kwenda kuwafaidisha au kuwanufaisha wenzetu wale ambao wako katika vyuo nya katil. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Mtemvu.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona ili niulize swalilmoja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yaliyotolewa ya swalila msingi imeonekana changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti kwa mwaka hadi mwaka, pamoja na ongezeko la bajeti tuliyoyelezwa, lakini ni ukweli kwamba, wanafunzi wenye sifa wanakuwa wengi na wale wanaokosa nafasi katika mwaka husika wengine wamekuwa wana kiu ya kuendelea na wananchi wamekuwa wakiwasaidia au jamii wanayoishi, sasa wakienda mwaka wa pili na watatu wanaendelea kukosa. Je, Serikali haioni inayo kila sababu sasa katika miaka inayofuatia wale wanafunzi waliosaidiwa katika njia mbalimbali wawaingize katika mwaka wa pili kabla hawajaendelea kuwachukua wengine?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalidogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, utaratibu huo upo. Sio kwamba, ukikosa mkopo katika mwaka wa kwanza basi unakuwa hu-*qualify*kwenye mwaka wa pili, *provided* ulikuwa umeomba katika ule mwaka wa kwanza. Unachofanya katika ule mwaka wa pili, unakuwa wewe sio mwombaji mpya, unakuwa uko katika dirisha la rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu huo upo Mheshimiwa Mbunge na tumekuwa tukiufanya na wanafunzi hao wamekuwa wakiwa-*absorbed*wakati wako mwaka wa pili ikiwa mwaka wa kwanza amekosa au mwaka wa tatu, hali ya mwaka wa kwanza na wa pili akiwa amekosa. Kwa hiyo, nikutoe wasiwasi na jambo hili tutaendelea nalo na ndivyo lilitivo.

MWENYEKITI: Swali la mwisho la nyongeza litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Tabasam.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasema usajili wa shule zetu, shule za msingi, sekondari na hadi vyuo vya kati hivi kama VETA, kumekuwa na masharti magumu sana katika Wizara ya Elimu. Kinachonishangaza hata shule za Serikali na zenyewe zinawekewa masharti magumu kupita kiasi, inatufanya sisi Wabunge ambao tuko vijijini huku wananchi wetu wanataka elimu, lakini tunapata zuvio kutoka katika Wizara ya Elimu.

Je, nini mpango wa Wizara ya Elimu kurahisisha usajili ili watu wengi waweze kusajili vyuo, kusajili shule zetu za msingi na sekondari? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tabasam anazungumzia suala la usajili. Niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, suala la usajili wa shule au taasisi hizi, linaanzia kule ambako shule ipo. Tuna watumishi wetu, wataalam wetu ambao wako kwenye maeneo hayo katika wilaya ambao wanakwenda kufanya ukaguzi kwenye maeneo hayo. Baada ya ukaguzi huo mara nyingi sana huwa wanaandika taarifa, ili kuweza kuangalia ile miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuanza kutoa elimu kama imefikiwa, basi tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi vile vile Mheshimiwa tabasam, hivi sasa Wizara iko mbioni kuhakikisha inakamilisha mfumo wa kufanya usajili kwa kupitia mfumo badala ya huu wa sasa wa kutumia makaratasi. Katika mfumo huo tunadhani vitu vingi sana vitakuwa ni rahisi na vyepesi na vitaondoa sana manung'uniko na mizunguko ile ambayo ilikuwa haina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kipindi hiki kifupi, tuendelee tu kuchukua hili wazo lake, lakini nimtoe wasiwasi, nakumbuka jana tulionana na nikamwambia leo tuonane tuweze kuangalia hayo maeneo yake ambayo anaona yana changamoto, lakini utaratibu kimsingi uko hivyo ni vitu tu vya kufuata utaratibu na fomu zile za kujaza. Tunaangalia zile *requirements* au yale mahitaji muhimu kwa ajili ya kuanza kutoa elimu kwa sababu, hatuwezi tu kusajili shule kwa sababu iko chini ya mti, ni lazima taratibu na miundombinu wezeshi iwepo. Hata hivyo, tunabeba wazo lake, tutakwenda kufanya maboresho kwenye eneo hili, lakini kwa vile mfumo unakwenda kuanza kufanya kazi, tunaamini maeneo mengi yatakwenda kuboreshwa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa *session* yetu ya maswali na majibu. Nitumie nafasi hii kuwashukuru wauliza maswali wote pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Msisitizo wetu bado ni kujibu maswali kwa ufupi, ili kutoa fursa kwa wauliza maswali wengi zaidi maana bado wachangiaji ni wengi sana, kwa hiyo, tunajaribu kukimbizana, lakini nafasi haitoshi.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wageni waliopo Bungeni leo asubuhi ni wageni watano wa Mheshimiwa Nape Moses Mnauye, Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaao ni viongozi wa Kampuni ya *Mwananchi Communication Limited (MCL)* kutoka Jijini Dar-es-Salaam, wakiongozwa na Mhariri Mtendaji wa Kampuni hiyo Ndugu Bakari Machumu. Ahsante, Ndugu Bakari Machumu, kiongozi wao, punga mkono pia; tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambaye pia ni mpiga kura wake kutoka Jimboni Longido, Mkoani Arusha, Ndugu Lokas Oloulu. Ahsante sana, mpiga kura wa Mheshimiwa Naibu Waziri wetu. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Issa Ali Mchungahela, na Mheshimiwa Khadija Taya, ambaao ni mawakili wa Taasisi ya *Best Nation Organization* kutoka Jijini Dar-es-Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Bertha Peter, sijui wako wapi? Ahsante sana wageni wa Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Khadija Taya, karibuni. (*Makofii*)

Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu na kufanya Marekebisho yatokanayo kwenye katika sheria nyingine tano, ili kukabiliana na changamoto katika Udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi wa Mwaka 2022 (*A Bill for an Act to Amend The Anti – Money Laundering Act and to make consequential amendment to five other laws for the purpose of addressing challenges in combating money laundering and countering financing of terrorism and countering the proliferation financing*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, anasema Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha Haramu wa Mwaka 2022 (*The Anti-Money Laundering Amendment Bill, 2022*) umeshasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni. Mara baada ya hatua hiyo na kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Spika, chini ya Kanuni ya 57(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Muswada huo sasa unaelekezwa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti, ili ufanyiwe kazi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika kwenye tamati ya kikao chetu cha leo, hivyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.00 Asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumaa,
Tarehe 4 Februari, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*